Sisi tu Watoto Wadogo

Msururu wa Mafunzo ya Biblia
Kwa Watoto wa Miaka 4-7
Na Sharon Kay Chatwell
Tafsiri ya Kiswahili na Ruth Mugeni

Krismasi

Somo la 1	Krismasi ni Nini?
Somo la 2	Ahadi ya Mfalme Mwokozi/ Safari ya kwenda Bethlehemu
Somo la 3	Hakuna Nafasi katika Nyumba ya Wageni
Somo la 4	Wachungaji na Malaika
Somo la 5	Wataalam wa Nyota (Mamajusi) kutoka mbali
Somo la 6	Kukimbilia Misri (Mungu Anamlinda Mtoto Yesu)

©2010, Sharon Kay Chatwell

Jinsi ya Kutumia Masomo haya

Kila somo:

- Limeundwa kwa ajili ya watoto, wenye umri wa miaka 4-7
- Linaweza kutumika pekee, au katika mfululizo wa masomo
- Linatokana na Biblia na linamheshimu Kristo

Kila somo lina sehemu 7:

Ushauri kwa Mwalimu: Maneno machache ya kutia moyo yaliyoandikwa haswa kwako, mwalimu atakayewasilisha somo. Pia utapata mistari kadhaa ya Biblia ya kuangalia kabla ya kufundisha somo.

Utakachohitaji: Orodha ya vitu utakavyovihitaji kuwasilisha somo. Pitia shughuli zilizopendekezwa ili uone ikiwa unahitaji vitu vyovyote kati ya ulivyochagua.

Hoja Kuu: Orodha ya hoja kuu zinazopaswa kutolewa wakati wa somo.

Mstari wa Kumbukumbu: Mstari wenye urefu unaofaa kwa umri wa watoto.
.

Somo: Mawazo ya hatua kwa hatua ya kuwasilisha hoja kuu kwa watoto. Tumia maneno yako mwenyewe, pamba na hadithi au mifano yako mwenyewe.

Maombi: Omba na watoto na uwaombee.

Shughuli Zinazopendekezwa: Michezo, ufundi, au shughuli ambazo huruhusu watoto kujibu Somo.

Vidokezo vya Kufundisha:

Soma ushauri kwa Mwalimu na uangalie **Mistari ya Biblia** iliyopendekezwa mapema, ili ukweli wa Biblia uwe ndani ya moyo wako kabla ya kuwafundisha watoto…. **Hii ndiyo siri ya kuwa mwalimu bora!**

Shughuli zilizopendekezwa ni **Mapendekezo tu.** Unaweza kufikiria michezo bora zaidi, ufundi, michoro au shughuli za kufanya na watoto. Ikiwa ndivyo, basi FANYENI! Kumbuka, una karama na talanta tofauti na mtu mwingine yeyote. Unaweza kuwa na rasilimali tofauti zinazopatikana. Omba Mungu akusaidie kuwa mbunifu katika njia za kuwafikia watoto na ujumbe wake**!**

Hoja kuu ni maoni ambayo yanapaswa kuwasilishwa kwa watoto wakati wa Somo. Hizi zimeelezwa kwa maneno rahisi sana, lakini ni dhana muhimu za kupendekeza.

©2010, Sharon Kay Chatwell

Watoto wanashangaza kwa kuwa wanaweza kuelewa mambo haya makubwa sana, hata ikiwa yametajwa kwa maneno rahisi sana. Labda hii ndio sababu Mwokozi wetu alituagiza kwamba Ufalme wa Mbinguni ni wa "wale walio kama hawa.**”**

Kila wakati unapofundisha watoto **UNAPASWA KUFANYA MAMBO HAYA 3:**

- WASIKILIZE
- OMBA nao na uwaombee
- Wakuone UKISOMA BIBLIA

SIKILIZA: Keti sakafuni na watoto na uwaulize jinsi wiki yao ilivyokuwa. Kisha SIKILIZA watoto mbalimbali wanapokuambia jambo lililo mioyoni au akilini mwao. Mara nyingi hii huchukua muda na juhudi, lakini watoto WANAHITAJI kuwa huru kukuambia juu ya matukio yao, ili uweze kuelewana nao.
.

OMBA: Mwanzoni mwa muda wenu pamoja, omba na watoto na uwaombee. Unaweza ukapenda kuombea baadhi ya changamoto zao au kwa ajili ya muda wenu pamoja. Omba Mungu akusaidie kufundisha somo ili wabarikiwe nalo. Fanya hivi kwa sauti. Watoto wanahitaji kujua kwamba unaomba na kwamba wanaweza pia kusali**.**
.

SOMA kutoka kwenye BIBLIA: Shikilia Biblia mikononi mwako au kwenye paja lako na waache watoto WAKUONE ukisoma mstari kutoka humo. Ni vizuri wajue kwamba kuna rejeo pale ambapo tunaweza kwenda kutafuta majibu ya Mungu. Ikiwa watakuona ukisoma Biblia, watajifunza kuwa wanaweza pia kufanya hivyo.

Mungu akubariki unapofanya kazi na watoto kuwasilisha kweli hizi kuu za kiroho kwao! Kazi yako shambani ilete mavuno mengi kwa ajili ya Ufalme wa Mungu!

Kwa upendo katika Kristo,

Sharon

©2010, Sharon Kay Chatwell

Krismasi ni nini Kwako?

Ushauri kwa Mwalimu: Ni furaha kubwa! Unapata kuongea na watoto wadogo kuhusu Krismasi inamaanisha nini kwao! Kuwa tayari kushangaa! Watakuwa na mengi ya kukuambia. Utasikia kuhusu tamaduni zote za Krismasi walizo nazo, na kile wanachotaka kwa ajili ya Krismasi.

Kisha sehemu ya kufurahisha zaidi ya yote! Unapata kuwaambia Krismasi ni nini! Unawaambia kuhusu ukweli kwamba Yesu, Mwana wa Mungu alizaliwa, na sababu ya kuwa na Krismasi ni kusherehekea kuzaliwa kwake!!

Utakachohitaji: Keki.

Hoja kuu: Wakati wa Krismasi tunasherehekea kuzaliwa kwa Yesu!
Maria alikuwa mama yake Yesu.
Mungu ni baba yake Yesu.

Maandiko: Luka 1:26-38 (Maria anaambiwa kumhusu Yesu)

Mstari wa Kumbukumbu: Luka 1:31 utampa jina Yesu.

Somo: **Sikukuu gani inakuja hivi karibuni?**

- Krismasi... Bila shaka, Krismasi!

Krismasi ina maana gani kwako?

- *(Sikiliza kila mtoto akisimulia kuhusu Krismasi. Huenda wakataka kukuambia jinsi wanavyosherehekea Krismasi nyumbani kwao. Sikiliza kwa makini. Sema mambo yanayo watia moyo.)*
- Mambo haya yote, tunayofanya na familia zetu, ni mambo mazuri yanayotusaidia kusherehekea Krismasi! Ninafurahi sana unasherehekea na familia yako na marafiki!

Leo nataka kukueleza sababu ya kuwa na Krismasi.

- Sababu ya kuwa na Krismasi ni kusherehekea kuzaliwa kwa Yesu!
- Yesu ni Mwana wa Mungu.
- Muda mrefu uliopita Yesu alizaliwa duniani, na ndiyo sababu tunasherehekea Krismasi. Ni siku ya kuzaliwa kwa Yesu!!

©2010, Sharon Kay Chatwell

Maria alikuwa mama yake Yesu.
- Maria lilikuwa jina la mwanamke aliyepata mtoto Yesu.
- Alikuwa mama yake Yesu.

Siku moja malaika alikuja kumwona Maria.
- Malaika alimwambia kwamba atapata mtoto.
- Mtoto angekuwa Mwana wa Mungu.
- Malaika alimwambia kwamba ampatie mtoto huyo jina, Yesu.

Mungu ni Baba wa Yesu.
- Mungu Baba alimwita Yesu “Mwana Wake wa Pekee.”
- Mungu ni baba yake Yesu.
- Mungu alitupenda sana na akamtuma Mwanawe hapa duniani.
- Tunasherehekea hili kwa kuwa na Krismasi kila mwaka!

Ombi: Tuombe na kumshukuru Mungu kwa kumtuma Mwanawe, Yesu!

Mungu mpendwa,
Asante kwa kuwa unatupenda.
Asante kwa kumtuma Mwanao, Yesu, kuwa hapa pamoja nasi.
Asante kwa Krismasi.
Tunakupenda. Amina.

Shughuli Zilizopendekezwa: (Chagua shughuli zinazokufaa zaidi!)

Kuwa na Sherehe ya Kuzaliwa!
- Mwimbie Yesu “Siku yenye furaha ya Kuzaliwa”
  - Imba "Siku ya Kuzaliwa yenye Furaha"!
- Kuwa na Keki (hiari)
  - **Ili kufurahia zaidi, endesha shughuli hii na vitafunio vyako.** Kuwa na keki na mshumaa juu yake ili kusherehekea Siku ya Kuzaliwa kwa Yesu. Mwambie mtu ambaye siku yake ya kuzaliwa iko karibu na Desemba 25 kuzima mshumaa.
- Zungumza zaidi kuhusu Kuzaliwa kwa Yesu
  - Waambie watoto kuwa imekuwa zaidi ya miaka 2000 tangu Yesu alipozaliwa. *(Hiyo itakuwa mishumaa mingi!!)* Eleza kwamba bado tunasherehekea kuzaliwa kwa Yesu kwa sababu lilikuwa jambo muhimu sana lililotukia!
- Cheza muziki wa Krismasi kwa utulivu chinichini wakati watoto wanakula na kucheza.
- Cheza baadhi ya michezo ya kawaida ya "sherehe ya siku ya kuzaliwa".

“Kupamba Keki”
Toa nakala za ukurasa wenye keki iliyo na jina la Yesu juu yake. Wape watoto kalamu za rangi na uwaelekeze "kupamba" keki kwa kuipaka rangi.

Yesu ni Mwana wa Mungu!

Ahadi ya Mfalme Mwokozi
(Safari ya kwenda Bethlehemu)

Ushauri kwa Mwalimu: Hebu fikiria msisimko ule ulikuwepo miaka hiyo yote iliyopita! Kila mtu alikuwa akimngoja Mwokozi na Mfalme aliyeahidiwa. Walijua ya kwamba siku moja hivi karibuni angezaliwa Bethlehemu. Licha ya hayo, wengi wao walikosa ujio wake. Hakuna aliyeonekana kumwona seremala mnyenyekevu na mkewe aliyeposwa wakisafiri kwenda Bethlehemu kuhesabiwa katika sensa. Lakini Mwana wa Mungu alikuwa karibu kuzaliwa, kama vile ilivyokuwa imetabiriwa katika maandiko… na kama vile malaika alivyowaambia Maria na Yosefu!

Wasaidie watoto kuona kwamba tunahitaji kutazama nyuma na kuona mambo yaliyotukia wakati wa kuzaliwa kwa Yesu. Tunahitaji kutambua kwamba Mungu alikuwa akitimiza ahadi yake ya kututumia Mfalme Mwokozi!

Utakachohitaji: Pamba, gundi, na kalamu za rangi kwa ajili ya shughuli iliyopendekezwa.

Hoja Kuu: Mungu alikuwa ameahidi kwamba Mwokozi angezaliwa Bethlehemu.
Malaika alizungumza na Maria na Yosefu.
Maria na Yosefu walisafiri hadi Bethlehemu.
Mwokozi, Mwana wa Mungu (Yesu) angezaliwa hivi karibuni!
Mungu alikuwa anatimiza ahadi zake!!

Maandiko: Mika 5:2 "Bethlehemu …kutoka kwako atatokea… yeye atakayekuwa mtawala katika Israeli, ambaye asili yake ni kutoka zamani, kutoka milele.

Mstari wa Kumbukumbu: Mathayo 2:1 …Yesu alizaliwa Bethlehemu …

Somo: **Krismasi inakaribia!!**

- Krismasi inakaribia! Tunasherehekea Krismasi kila mwaka! Kwa nini tunasherehekea Krismasi *(Subiri majibu.)*
- Hiyo ni sawa! Krismasi ni wakati tunasherehekea kuzaliwa kwa Yesu!
- Leo tutazungumzia KWA NINI Yesu alizaliwa.

Mungu alitoa ahadi ya kumtuma Mfalme Mwokozi.

- Muda mrefu uliopita Mungu alitoa ahadi ya kututumia Mwokozi.
- Neno Mwokozi linamaanisha “mtu anayeokoa.”
- Mtu huyo alikuwa Yesu, Mwana wa pekee wa Mungu!

©2010, Sharon Kay Chatwell

Watu walikuwa wakisubiri ahadi itekelezwe.

- Mtu akiniahidi, nataka atimize! Je! wewe sivyo*? (Subiri majibu).* Huwasubiri watimize ahadi yao. Natarajia wafanya hivyo!
- Watu walimngoja Mungu kutimiza ahadi yake. Walijua kwamba Mwokozi angezaliwa mahali paitwapo Bethlehemu. Walingoja na kutazama. Lakini Mungu aliwafanya wangojee kwa muda mrefu sana. Na baadhi yao walisahau kuendelea kutazama!!

Malaika anazungumza na Maria na Yosefu.

- Maria alikuwa msichana mzuri sana aliyeishi zamani hizo.
- Siku moja malaika kutoka kwa Mungu alimtembelea Maria.
- Malaika alimwambia Maria kwamba atapata mtoto maalum.
- Mtoto angekuwa Mwana wa Mungu. (Mwokozi)
- Baadaye, malaika alimwambia Yosefu pia. (Yosefu alikuwa mtu ambaye angekuwa mume wa Maria.)
- Malaika aliwaambia wampe mtoto jina Yesu.

Maria na Yosefu walisafiri hadi Bethlehemu

- Maria na Yosefu wote waliishi mahali paitwapo Nazareti.
- Siku moja, mtawala wa nchi (Kaisari) aliamuru kila mtu arudi katika mji wake, ili ahesabiwe.
- Hivyo basi Maria alisafiri pamoja na Yosefu safari ndefu hadi Bethlehemu, ambao ulikuwa mji wa asili wa familia yake.

Mungu hutimiza ahadi zake.

- Yesu alizaliwa katika mji mdogo unaoitwa Bethlehemu, kama vile Mungu alivyokuwa ameahidi miaka mingi kabla!!
- Wakati wowote Mungu anapotoa ahadi, Yeye huitimiza!!
- Mungu aliahidi kutuma Mwokozi, na alifanya hivyo! Yesu, Mwana wa pekee wa Mungu, ndiye Mwokozi aliyeahidiwa!
- Mungu daima hutimiza ahadi zake, haijalishi ni kubwa au ndogo kiasi gani.

Ombi: Tuombe na kumshukuru Mungu kwa kutimiza ahadi yake ya kumtuma Mwokozi.

Mungu mpendwa,
Asante kwa kutimiza ahadi zako.
Asante kwa kumtuma Mwanao, Yesu, kuwa Mwokozi wetu.
Asante kwa Krismasi.
Tunakupenda. Amina.

Shughuli Zinazopendekezwa: (Chagua shughuli zinazokufaa zaidi!)

<u>Mabawa ya malaika yaliyotengezwa kwa pamba</u>

Kwa shughuli hii, tengeneza nakala za ukurasa wa mbawa za malaika na umpe kila mtoto. Wakumbushe watoto kwamba malaika alikuja na kumtembelea Maria na kisha akamtembelea Yosefu kuwaambia kuhusu mtoto Yesu! Wape watoto kalamu za rangi,

gundi, na pamba. Kwanza, waambie watoto wapake rangi uso wa malaika, nywele, mikono na vazi la malaika. ***(USIPAKE rangi kwenye mbawa za malaika… au gundi inaweza isishike vizuri!) Kisha, waruhusu watoto wachovye ncha ya mipira ya pamba kwenye gundi na kuiweka kwenye mbawa za malaika*** *(DOKEZO: Mimina gundi kidogo kwenye kifuniko kidogo cha plastiki. Hiyo inafanya kazi vizuri kwa kuchovya pamba!)*

KUMBUKA: Ukizitunza hizi siku ya ziada au zaidi, unaweza kufanya mapambo mazuri ya mti wa Krismasi.

Imba Nyimbo za Krismasi

Usiku Mtakatifu

Usiku, Mtakatifu,
Wengine, walala,
wakeshao ni Yosefu tu
na Maria waliomlinda.
Yesu mwana mzuri
Yesu mwana mzuri.

Furaha kwa ulimwengu

Furaha kwa ulimwengu!
Bwana amekuja;
Nyote mkaribisheni,
Mioyo yenu na mpeni;
Wote wamshangilie,
Wote wamshangilie,
Na wote, na wote wamshangilie..

Twawatakia krismasi njema,

Twawatakia krismasi njema,
Twawatakia krismasi njema,
Twawatakia krismasi njema,
mwaka mpya mwema!

Heri katika siku yako ya kuzaliwa

Afya njema na furaha
Afya njema na furaha
Afya njema na furaha mpendwa Yesu
Afya njema na furaha mpendwa Yesu

Jifunze Mstari wa Kumbukumbu

Mstari wa Kumbukumbu ni Mathayo 2:1 …Yesu alizaliwa Bethlehemu.....

Tumia njia hii:

Sema “Yesu alizaliwa Bethlehemu”
(Acha watoto warudie… kama wewe.)
Sema "Yesu alizaliwa _____"
(Waambie watoto wajaze nafasi iliyo wazi.)

(Sasa jaribu kurudia vifungu vya maneno kwa kutumia mkazo tofauti wa sauti au unapofanya mambo tofauti. Waambie watoto wayarudie kama wewe.)

Rudia kwa sauti kubwa, laini, kusimama, kukaa, kugeuka, na kusimama kwa mguu mmoja.

Rudia na kuruka juu neno "Bethlehemu" linapotajwa

Je! kila mtu anajua sasa? Nafikiri wanajua. Nafikiri hata watu katika darasa lililo karibu na wewe wanajua kwa sasa! Hongera sana!!

©2010, Sharon Kay Chatwell

"Mungu Hutimiza Ahadi Zake!"

Kuzaliwa kwa Yesu Kulitabiriwa - Luka 1:26-38

Hakuna Nafasi katika Nyumba ya Wageni!

Ushauri kwa Mwalimu: Ni jambo zuri kuweza kuwafundisha watoto kuhusu mambo yaliyotukia wakati wa kuzaliwa kwa Yesu. Ingawa Yesu ni Mwana wa Mungu, na Mwokozi aliyeahidiwa na Mfalme, Yeye hakuzaliwa katika jumba la kifahari au katika jiji kuu la Yerusalemu. Anazaliwa katika zizi la ng'ombe katika mji mdogo unaoitwa Bethlehemu. Lakini Bethlehemu palikuwa mahali pa maana sana. Ulikuwa ni mji wa asili wa babu Yake, Daudi. Daudi alikuwa ameanza maisha akiwa mchungaji, lakini baadaye Mungu alimchagua awe mfalme. Daudi aliitwa “mtu anayeupendeza moyo wa Mungu.”

Utakachohitaji: Vipande kadhaa vya karatasi vilivyo na alama ya “O” na kipande kimoja cha karatasi chenye alama ya “X” kwa ajili ya mchezo..

Hoja Kuu: Mwokozi alipaswa kuzaliwa hivi karibuni.
Maria na Yosefu walisafiri hadi Bethlehemu.
Hakukuwa na nafasi kwa ajili yao katika nyumba ya wageni!
Mtoto Yesu alizaliwa katika zizi la ng'ombe huko Bethlehemu.

Maandiko: Luka 2:4-7 Hivyo Yosefu akapanda kutoka mji wa Nazareti ulioko Galilaya kwenda Uyahudi, mpaka Bethlehemu, mji wa Daudi, kwa sababu yeye alikuwa wa ukoo na wa nyumba ya Daudi. Alikwenda huko kujiandikisha pamoja na Maria, ambaye alikuwa amemposa naye alikuwa mjamzito. Wakiwa Bethlehemu, wakati wa Maria wa kujifungua ukawa umetimia, naye akamzaa mwanawe, kifungua mimba. Akamfunika nguo za kitoto na kumlaza katika hori ya kulia ng’ombe, kwa sababu hapakuwa na nafasi katika nyumba ya wageni.

Mstari wa Kumbukumbu: Luke 2:7 … hapakuwa na nafasi katika nyumba ya wageni.

.

Somo: **Krismasi itawadia hivi karibuni!**

- Sote tunatazamia Krismasi.
- Ninafuraha! Wewe je? (*Subiri majibu*.)
- Inafurahisha kufikiria kuhusu Krismasi kuja hivi karibuni!
- Pia napenda kukumbuka mambo yote ya kusisimua yaliyotukia muda mrefu uliopita kwenye Krismasi hiyo ya kwanza, Yesu alipozaliwa!

Mwokozi alipaswa kuzaliwa hivi karibuni!

- Malaika alikuwa amewatembelea Maria na Yosefu na kuwaambia kwamba mtoto Yesu angezaliwa.
- Yesu alikuwa Mwokozi na Mfalme aliyeahidiwa!

©2010, Sharon Kay Chatwell

Maria na Yosefu walisafiri hadi Bethlehemu.

- Siku moja, kabla ya Yesu kuzaliwa, mtawala wa nchi (Kaisari) alisema kwamba kila mtu alipaswa kusafiri hadi mji wa nyumbani wa familia yake ili kuhesabiwa.
- Familia ya Yosefu ilitoka Bethlehemu.
- Maria na Yosefu walilazimika kusafiri umbali mrefu kwenda Bethlehemu.

Hakukuwa na nafasi kwa ajili yao katika nyumba ya wageni!

- Walipofika, kulikuwa na watu wengi Bethlehemu!!
- Maria na Yosefu walitafuta mahali pa kukaa, lakini hapakuwa na nafasi katika nyumba ya wageni!!
- Kwa hiyo, Maria na Yosefu walikwenda kukaa katika zizi la ng'ombe, ambamo wanyama waliwekwa.

Mtoto Yesu alizaliwa katika zizi la ng'ombe huko Bethlehemu!

- Wakiwa huko mtoto Yesu alizaliwa!!
- Maria alimfunika mtoto Yesu kwa vitambaa na kumlaza katika hori ya kulia ng'ombe. (Hori lilikuwa sanduku la mbao lililojaa nyasi kwenye zizi.)
- Mwokozi wa ulimwengu, Mwana wa Mungu (Yesu) alikuwa amezaliwa!
- Ni jambo la ajabu sana! Mungu asifiwe!!

Mfalme katika mazingira duni

- Unafikiri wafalme wengi wanazaliwa wapi? (*Subiri majibu*.)
- Hiyo ni sawa. Wafalme wengi huzaliwa katika majumba ya kifahari au majumba ya kifalme.
- Inachekesha, sivyo? Ingawa Yesu ni Mwokozi na Mfalme wa ulimwengu wote, Hakuzaliwa katika jumba la kifahari au la kifalme.
- Mungu hakutaka vitu hivyo kwa ajili ya Mwanawe.
- Yesu alizaliwa katika zizi la ng'ombe katika jiji la babu yake, Mfalme Daudi, ambaye alimpenda Mungu sana.
- Hili lilikuwa muhimu sana kwa Mungu! Inaweza kuwa muhimu kwetu pia! Mtu anapokuwa mnyenyekevu, inamaanisha ni rahisi kumkaribia.
- Yesu anataka tujue kwamba tunaweza kuja kwake wakati wowote.
- Njia moja tunaweza kuja kwake ni kwa kuomba.

Ombi: Tuombe na kumshukuru Mungu kwa kumtuma Yesu kwetu.

Mungu mpendwa,
Asante kwa kumtuma Mwanao, Yesu, kuwa Mwokozi wetu.
Asante kwa kuwa alikuja kwetu kwa unyenyekevu sana.
Asante kwa Krismasi.

Tunakupenda. Amina.

Shughuli Zinazopendekezwa: (Chagua shughuli zinazokufaa zaidi!)

“Mchezo”
Huu ni mchezo mzuri! Darasa liigize hadithi ya Maria na Yosefu wakisafiri kwenda Bethlehemu. Watu wawili waigize sehemu za Maria na Yosefu. Wabebe mizigo na kusafiri kuzunguka chumba ili kufika Bethlehemu. Watu wengine ni wakaaji wa Bethlehemu. *(Watu hawa kila mmoja achague kipande cha karatasi chenye "X" au "O" juu yake.)* **KANUNI: Kuwa na "X" moja tu kwa kila kikundi. Usimwambie mtu yeyote ikiwa una X au O!** Waambie watoto waenee kuzunguka chumba. Maria na Yosefu wanaenda kutoka mtu hadi mtu wakiomba mahali pa kukaa. Kila mtu aliye na "O" anawaambia "Hakuna nafasi katika nyumba ya wageni!" Hatimaye wanampata mtu aliye na “X” kwenye karatasi. Mtu huyo anawaambia kwamba wanaweza kukaa kwenye zizi. Maria na Yosefu wana furaha! Cheza tena na watu wengine wakiigiza sehemu za Maria na Yosefu.

Hori ni nini?
Hakuna anayejua hori ni nini, isipokuwa aliyefundishwa na mtu mwingine. Jadili kuwa hori lilikuwa sanduku la mbao ambalo lilikuwa limejaa majani ambayo wanyama walitumia kula chakula chao. Kwa kuwa Maria na Yosefu walikuwa ndani ya zizi la ng’ombe, kulikuwa na hori karibu kwa sababu wanyama walikuwa wakila kutoka humo kila siku.

Unda hori: Tumia karai safi ya kufulia. Jaza kwa taulo au blanketi. (Unaweza kutumia nyasi, ikiwezekana.) Tafuta mdoli wa watoto. Mfunge na kitambaa chepesi na uweke mdoli kwenye hori. Waruhusu watoto kuchukua zamu kumfunga mtoto na kumweka kwenye hori. Weka blanketi ndani na nje mara chache. *Hakikisha kwamba watoto wanambeba mdoli kwa upole na kwa heshima, kwa kuwa anawakilisha mtoto Yesu.*

Imba Wimbo wa Mzee Fulani
Zizi humaanisha wanyama …… Imba wimbo wa “Mzee Fulani” na uwaruhusu watoto kutaja majina ya wanyama mbalimbali. Sitisha kidogo wakati wa wimbo ili kutoa muda wa kutosha wa kufanya sauti zote zinazofaa za wanyama! Wataipenda hii! Imba KWA SAUTI!!

MZEE FULANI
Mzee fulani anayo shamba …
E-I-E-I-O
Na kwenye shamba anao ng’ombe …
(Simama na uulize ... "Nini?" Subiri jibu, rudia neno, kisha uendelee …)
E-I-E-I-O
Wana _____ _____ hapa,
Na _____ _____ pale,
Hapa _____,
Pale_____,
Kote _____ _____!
Mzee fulani anayo shamba…

E-I-E-I-O!!

Ukurasa wa Kuchorea

Tumia ukurasa wa kupaka rangi uliotolewa wa zizi na hori. Tengeneza nakala kwa kila mtoto na uwape kalamu za rangi. Wape watoto muda wa kupaka rangi ukurasa kwa uangalifu. Wahimize wachore baadhi ya wanyama karibu na zizi. Ni wanyama wa aina gani wanaweza kuwa huko? (Kondoo, mbuzi, ng'ombe, farasi au punda, kuku, nk).

.

Mtoto Yesu alizaliwa katika zizi
na kuwekwa kwenye hori.

Wachungaji na Malaika

Ushauri kwa Mwalimu: Haikuwa muda mrefu uliopita, ukifikiri juu yake. Bila shaka, imekuwa zaidi ya miaka 2000… lakini… Bethlehemu bado ipo… na vilima vya Yudea, ambako wachungaji walikuwa "wakichunga mifugo yao usiku," bado ni vile vile. Milima ya chini imefunikwa na mawe makubwa na nyasi kavu. Kuna miti michache, ikiwa ipo, ambayo ina maana kwamba wakati wa usiku hata kundi la wachungaji lenye usingizi lingeweza kuona kila nyota angani (bila kutaja "jeshi la mbinguni" linalomsifu Mungu!) Hebu fikiria maajabu hayo yote! Wachungaji waliotembelewa na malaika waliotangaza kuzaliwa kwake kwa ulimwengu wote! "Maana leo katika mji wa Daudi amezaliwa kwa ajili yenu, Mwokozi, ndiye Kristo Bwana." Ni kama imetokea jana tu!

Utakachohitaji: Tangazo la kuzaliwa la kuonyesha wakati wa somo.
Mavazi kwa ajili ya mchezo wa kuigiza. Tazama mchezo wa kuigiza ili upate wazo kuhusu mavazi.
Kalamu za rangi, au mapambo mengine kulingana na chaguo la shughuli.

Hoja Kuu: Mwokozi, Yesu, alizaliwa Bethlehemu.
Malaika watangazia wachungaji Habari Njema.
Wachungaji walikuja kumwabudu Yesu.

Maandiko: Luka 2:8-20 (Malaika wanawatokea wachungaji.)

Mstari wa Kumbukumbu: Luka 2:14 "Atukuzwe Mungu juu mbinguni…"

Somo: **Krismasi inakaribia!**

- Tunakuwa na Krismasi kila mwaka kusherehekea kwamba Yesu, Mwokozi, alizaliwa!!
- Hebu tuzungumze kuhusu Krismasi ya kwanza kabisa!

Krismasi ya kwanza…

- Maria na Yosefu walikuwa wamesafiri kwenda Bethlehemu.
- Hakukuwa na nafasi katika nyumba ya wageni, lakini hatimaye walipata mahali pa kukaa kwenye zizi.
- Mtoto Yesu alizaliwa wakiwa huko.
- Maria alimfunga mtoto kwa vitambaa na kumlaza katika hori la ng'ombe.

Tangazo la Kuzaliwa

- Mtoto mchanga anapozaliwa, mara nyingi wazazi hutuma tangazo la kuzaliwa. *(Onyesha tangazo la kuzaliwa.)*
- Linaeleza wakati mtoto alizaliwa, na yote kuhusu mtoto.
- Mungu ni baba ya Yesu. Alitaka ulimwengu wote ujue kwamba Mwanawe wa Pekee alikuwa amezaliwa Bethlehemu!
- Mungu alituma tangazo la ajabu la kuzaliwa!

©2010, Sharon Kay Chatwell

- Lakini Mungu hakutuma matangazo ya karatasi. Mungu alituma malaika!

Malaika wanatembelea Wachungaji

- Wachungaji ni watu wanaochunga makundi ya kondoo.
- Usiku huo kulikuwa na wachungaji wakiwachunga kondoo wao.
- Mungu alimtuma malaika kuzungumza na wachungaji.
- Hivi ndivyo malaika aliwaambia wachungaji: “Msiogope. Kwa maana tazama nawaletea habari njema za furaha itakayokuwa kwa watu wote. Leo katika mji wa Daudi kwa ajili yenu amezaliwa Mwokozi, ndiye Kristo Bwana. Hii ndiyo itakayokuwa ishara kwenu: Mtamkuta mtoto mchanga amefunikwa nguo za kitoto na kulazwa katika hori ya kulia ng’ombe.
- Ghafla mbingu ikajaa malaika wakiimba sifa kwa Mungu. Waliimba “Atukuzwe Mungu juu mbinguni, na duniani iwe amani kwa watu aliowaridhia.”

Wachungaji walikuja kumwabudu Yesu.

- Wachungaji walitaka kumuona Mwokozi!
- Wakafika Bethlehemu (mji wa Daudi).
- Walimkuta mtoto mchanga amevikwa vitambaa na amelala horini… Kama walivyoambiwa na malaika!
- Walimwabudu mtoto mchanga, Yesu, na kumsifu Mungu!
- Tunaweza kumsifu Mungu pia! Hebu tuseme maneno ambayo malaika walisema; “Utukufu kwa Mungu juu! (*Waambie watoto warudie.*)

Ombi: Tuombe na kumshukuru Mungu kwa kumtuma mtoto Yesu!

Mungu mpendwa,
Asante kwa kumtuma mtoto Yesu.
Asante kwamba Yeye ni Mwana wako na Mwokozi wetu.
Asante kwa Krismasi.
Tunakupenda. Amina.

Shughuli Zinazopendekezwa: (Chagua shughuli zinazokufaa zaidi!)

Igiza mchezo wa Krismasi uliosimuliwa

Watoto wadogo hivi wanahitaji sana kuigiza sehemu za hadithi ya Krismasi ili waweze kuelewa yote yaliyotokea. Tumia maandishi haya yaliyosimuliwa ili kuwasaidia kuigiza sehemu za wachungaji, malaika, Maria na Yosefu.

Mavazi ya Kuigiza:
Watoto wadogo hivi wanafurahishwa na mavazi rahisi sana. Kwa mfano vipande vikubwa vya nguo (takriban futi 4x4 za mraba) hutengeneza kofia nzuri. Ukikata shimo katikati (kwa vichwa vya watoto kupitia) pia hutengeneza mavazi mazuri. Tumia kipande chembamba cha kitambaa kama mkanda. Tengeneza hori kutoka kwa karai ya nguo/kuogea na taulo au blanketi.

KUMBUKA: Baada ya kukusanya sanduku langu la kwanza la mavazi, niliihifadhi kwa ajili ya michezo ya Krismasi za siku zijazo. Imekuwa ya manufaa mara nyingi! Kwa miaka mingi niliongeza kwenye mkusanyiko. Sasa, ninaweza kuwavisha wachungaji wachache na "jeshi" zima la malaika! Tunza mavazi yako!!

WACHUNGAJI NA MALAIKA –MCHEZO WA KUIGIZA

MSIMULIZI:

Maria na Yosefu walisafiri hadi Bethlehemu. Walipofika huko, kulikuwa na wageni wengi hivi kwamba hakukuwa na nafasi katika nyumba ya wageni.

Mlinzi wa nyumba ya wageni aliona uhitaji wao mkubwa na akawaambia kwamba wangeweza kukaa kwenye zizi.

Wakiwa huko, Maria alimzaa mtoto wake, Yesu. Akamfunga sanda na kumlaza horini.

Karibu na hapo palikuwa na wachungaji huko kondeni, wakichunga makundi yao usiku.

Mara malaika wa Bwana akawatokea! Na waliogopa sana!

Lakini malaika akawaambia, "Msiogope. Ninawaletea habari njema ya furaha kuu itakayokuwa kwa watu wote. Leo katika mji wa Daudi amezaliwa kwa ajili yenu Mwokozi, ndiye Kristo Bwana. Hii itakuwa ishara kwenu: Mtamkuta mtoto mchanga amevikwa nguo na amelala horini."

Kisha malaika akajiunga na jeshi la mbinguni likisema “Utukufu kwa Mungu juu mbinguni na duniani amani kwa watu aliowaridhia.”

Baada ya malaika kuondoka, wachungaji walijisemea. Twendeni mjini tuone jambo hili ambalo Bwana ametuambia.

Na hivyo wakaenda na kumkuta mtoto Yesu. Alikuwa amevikwa vitambaa na kulazwa horini, kama vile malaika alivyowaambia!

Wachungaji walipompata mtoto Yesu, walimwabudu.

Wachungaji walimsifu Mungu kwa sababu walifurahi sana kwamba Mwokozi alikuwa amezaliwa!

Tunafurahi pia! Na tunaweza kumsifu Mungu kama vile malaika na wachungaji walivyofanya!!

KILA MTU:

Utukufu kwa Mungu juu!

MWISHO

Tangazo la Kuzaliwa la Mbinguni

Mungu alitangaza kuzaliwa kwa Mwanawe wa Pekee kwa njia ya ajabu: Alituma malaika kuzungumza na wachungaji! Pamba Tangazo hili la Mbinguni la Kuzaliwa kwa Mtoto Yesu au ubuni lako mwenyewe. Kata na kuiweka kwenye karatasi ngumu.

Amezaliwa leo katika Jiji la Daudi, Mwokozi ambaye ni Kristo Bwana

"Utukufu kwa Mungu aliye juu

Na duniani

AMANI

Heri njema kwa Watu!"

Jina: *Yesu, Mwana wa Mungu, Mwokozi, Kristo Bwana*

Lini: *Krismasi ya kwanza*

Wapi: *Bethlehemu… zizi… hori*

Wachungaji walikuja kumwabudu mtoto Yesu.



Wasaidie wachungaji kumpata mtoto Yesu. Chora katika nyuso zao, mikono na miguu, na upake rangi mavazi yao.

Wataalam wa Nyota (Mamajusi) kutoka Mbali

Ushauri kwa Mwalimu: Kwa mfano tuseme wewe ni mtaalamu. Unasoma nyota. Kwa kuongezea una ujuzi wa kufanya kazi ya hesabu na umesoma maandiko ya kale ya Kiebrania. Unajua kwamba siku moja Mwokozi aliyeahidiwa atazaliwa kwa Wayahudi. Usiku mmoja unaona nyota mpya angani, na ghafla unagundua: Amekuja!!

Inasisimua jinsi gani! Kama mwalimu, unapata kuwasaidia watoto kutambua ajabu ya kuja kwa Masiya! Wataalamu wa nyota lazima iwe walihisi mshangao na msisimko. Walitambua kwamba Mfalme aliyeahidiwa wa Wayahudi alikuwa amezaliwa, na wakamtafuta. Walisafiri umbali mrefu, wakampelekea zawadi, na wakamwabudu!

Utakachohitaji: Ukurasa wa kuchorea kwa kila mtoto. Gundi, mapambo ya rangi ya dhahabu, na gazeti. Mavazi kwa ajili ya kuigiza (Si lazima). Tazama mchezo wa kuigiza ili ikusaidie kuchagua mavazi ya kuigiza.

Hoja Kuu: Wale wataalam wa nyota waliona nyota angani.
Walijua kwamba nyota ilimaanisha kwamba Mwokozi alikuwa amezaliwa.
Walienda kumtafuta Mwokozi.
Walipompata walimpa zawadi na kumwabudu.
Yesu ni zawadi ya Mungu kwetu!

Maandiko: Mathayo 2:1-12

Mstari wa Kumbukumbu: Mathayo 2:2 nasi tumekuja kumwabudu.

Somo: **Krismasi ni ya furaha!**

- Krismasi ni ya furaha! Na Krismasi ni ya kusisimua! Je, ni sehemu gani ya kufurahisha zaidi (ya kusisimua) kuhusu Krismasi? *(Subiri majibu.)*
- Kweli! Moja ya sehemu ya kufurahisha zaidi kuhusu Krismasi ni kupata zawadi!! Ninapenda kupokea zawadi!! Je wewe?!
- Unaweza kuniambia kwa nini tunapeana zawadi wakati wa Krismasi? *(Subiri majibu.)*
- Ndiyo, tunapeana zawadi kwa sababu tunapendana na kwa sababu tunataka kuwafurahisha watu tunaowapenda. Lakini kuna sababu nyingine pia!
- Tunatoa zawadi wakati wa Krismasi kwa sababu tunakumbuka kwamba wataalam wa nyota walimpa mtoto Yesu zawadi walipompata.

Wale wataalam wa nyota waliona nyota angani.

- Wakati Yesu alipozaliwa, kulikuwa na wataalam wa nyota walioishi katika nchi jirani na ambao walichunguza nyota.

- Siku moja wataalam wa nyota waliona nyota mpya kabisa mbinguni.
- Walijua ilimaanisha kwamba Mwokozi alikuwa amezaliwa!
- Wataalam wa nyota walifurahi sana! Walijua kwamba Mfalme wa Wayahudi alikuwa amezaliwa, kama tu Mungu alivyoahidi!

Wataalam wa nyota walikwenda kumtafuta Mwokozi.

- Wataalam wa nyota walisafiri umbali wote kutoka nchi zao kuja kumwona mtoto Yesu.
- Kwa kuwa walikuwa wanatafuta mfalme, kwa kawaida walienda katika mji mkuu (Yerusalemu) ili kuona kama alikuwa huko.
- Waliuliza kwenye lango la jiji kuu “Yuko wapi Yeye aliyezaliwa Mfalme wa Wayahudi?”
- Waliambiwa kwamba angezaliwa Bethlehemu.
- Kwa furaha, Bethlehemu haikuwa mbali sana!

Wataalam wa nyota walimpata Yesu!

- Wataalam wa nyota walifuata nyota hadi Bethlehemu na kumpata Yesu!
- Walipompata waliinama na kumwabudu.
- Kisha wakampa zawadi (dhahabu, uvumba, na manemane.)
- Yesu alikuwa Mwokozi aliyeahidiwa na Mfalme wa Wayahudi.

Tunatoa zawadi.

- Kwa hiyo, sasa tunapeana zawadi wakati wa Krismasi kwa sababu tunakumbuka zawadi ambazo wataalam wa nyota walimpa mtoto Yesu.
- Pia tunakumbuka kwamba zawadi bora kuliko zote ni Yesu!!
- Yesu ni zawadi ya Mungu kwetu!

Ombi: Tuombe na kumshukuru Mungu kwa kutupa zawadi hii ya ajabu!

Mungu mpendwa,
Asante kwa kutupatia zawadi hii nzuri!
Asante kwa kututumia Yesu, Mwana wako wa Pekee.
Asante kwa Krismasi.
Tunakupenda. Amina.

Shughuli Zinazopendekezwa: (Chagua shughuli zinazokufaa zaidi!)

<u>Shughuli ya Nyota inayongaa</u>
Tandika magazeti juu ya meza. Ruhusu watoto kuweka gundi kwenye nyota iliyo katika karatasi ya shughuli. Nyunyiza na mapambo yenye rangi ya dhahabu. Iruhusu kukauka!

<u>Igiza mchezo wa Krismasi wa kusimuliwa</u>
Watoto wachanga hivi wanahitaji sana kuigiza sehemu za hadithi ya Krismasi ili waweze kuelewa yote yaliyotokea. Tumia maandishi yaliyosimuliwa kwa watoto wa umri wa shule ya awali ili kuwasaidia kuigiza sehemu za wafalme, pamoja na Maria na Yosefu.

Mavazi ya kuigiza:
Watoto wadogo hivi wanafurahia mavazi rahisi sana. Kwa mfano: Vipande vikubwa vya nguo (takriban futi 4x4 za mraba) hutengeneza kofia bora. Ukikata shimo katikati (Ili vichwa vya watoto kupitia) pia hufanya mavazi mazuri. Tumia vipande vyembamba vya kitambaa au mikanda kiunoni. Tengeneza hori kutoka kwa karai ya kufulia iliyofunikwa na blanketi au taulo.
Uwe na mwanasesere (Mdoli) wa kumwakilisha mtoto Yesu. Hakikisha watoto wanamshika mdoli huyo kwa upole na kwa heshima, kwa kuwa anawakilisha mtoto Yesu.

©2010, Sharon Kay Chatwell

WATAALAMU WA NYOTA (MAMAJUSI) KUTOKA MBALI – MCHEZO WA KUIGIZA WA KRISMASI

MSIMULIZI:

Yesu alipozaliwa, wataalam fulani wa nyota (mamajusi) walioishi mbali waliona nyota mpya mbinguni. Walifurahi sana!

Wale wataalam walijua kwamba nyota mpya ilimaanisha kwamba Mwokozi alikuwa amezaliwa!!

Walitaka kumwona. Kwa hiyo wakaifuata ile nyota ili wampate.

Wataalam wa nyota walijua kwamba mtoto huyo alikuwa Mfalme wa Wayahudi aliyeahidiwa.

Kwa kuwa walikuwa wanatafuta mfalme, walienda kwenye mji mkuu. Wale wataalam wa nyota wakasimama katika malango ya mji mkuu na kusema, “Yuko wapi yeye aliyezaliwa Mfalme wa Wayahudi?” “Tumekuja kumwabudu Yeye!”

Waliambiwa kwamba Mwokozi angezaliwa Bethlehemu.

Wataalam wa nyota walifurahi! Bethlehemu haikuwa mbali sana! Hivi karibuni wangemwona!

Wakaifuata ile nyota mpaka Bethlehemu, wakamkuta mtoto mdogo, Yesu.

Walipompata waliinama na kumwabudu.

Kisha wakafungua hazina zao na kumpa zawadi: dhahabu, uvumba na manemane.

Wataalam wa nyota walifurahi sana kumpata Yesu! Tunaweza kufurahi pia!

Tunatoa zawadi wakati wa Krismasi kwa sababu tunakumbuka zawadi ambazo wataalam wa nyota walimletea Yesu.

Pia tunajua kwamba Yesu ni zawadi ya Mungu kwetu!

Wataalam wa nyota walimwabudu Yesu na sisi pia tunaweza! Kama tu wataalam wa nyota tunaweza kusema sote.....

KILA MTU:

Tumekuja kumwabudu!

MWISHO

©2010, Sharon Kay Chatwell



Nyota
Maalum
Iling'aa
Angani
Usiku
Huo!

Kukimbilia Misri
(Mungu Anamlinda Mtoto Yesu)

Ushauri kwa mwalimu: Katika somo hili watoto wataigiza Safari ya kukimbilia Misri... **mpaka kwenye hema!** *(Hii lazima iwe mojawapo ya shughuli BORA ZAIDI inayopendwa na watoto SANA!)* Watoto watajifunza kwamba Mungu alimtuma malaika kumwonya Yosefu juu ya hatari, na kwamba Yosefu alifanya jinsi Mungu alivyosema afanye! BWANA alimlinda mtoto Yesu na kumweka salama! Hili ni somo kuu la kufanya BAADA ya Krismasi!

KUMBUKA: Sio lazima ujadili "Machinjo ya Wasio na Hatia" na watoto. Walakini itasaidia ikiwa unaifahamu hadithi hiyo. Inasaidia kutambua ni kiasi gani cha hatari waliyokuwa ndani yake.

Walimu Pekee: Fikiria Yosefu. Kuna giza. Moyo wake unadunda. Ameamka tu kutoka kwenye ndoto ya kutisha. Anamwamsha Maria na kumwambia avae haraka. Ni lazima wamchukue mtoto na kukimbilia Misri. Mungu amemwambia kuna wanaume wanakuja kujaribu kumuua mtoto! Wanakusanya vitu vyao (pamoja na zawadi walizopewa hivi punde na mamajusi.) Wanaondoka kungali giza, labda hata huku moyo wa Yosefu ungali unadunda. Wanatoweka gizani na kukaa kimya. Nyuma yao watasikia vilio vya mbali. Ni “Raheli akiwalilia watoto wake… kwa sababu hawapo tena.”

Utakachohitaji: Vifaa vya kusaidia kutengeneza "hema" katika chumba. *(Kwa mfano: blanketi kadhaa au shuka za kuweka juu ya meza ndefu.)* Vitafunio, kama vile mkate na maji, vya kula katika hema. Vitu vingine ambavyo unaweza kubeba katika safari. *(Kwa mfano: chupa za maji, blanketi, mkoba, nk.)*

Hoja kuu: Mungu alimtuma malaika kumwonya Yosefu kuhusu hatari fulani!
Mungu aliwaambia wakimbilie Misri.
Yusufu alifanya kile ambacho Mungu alisema.
BWANA alimwangalia Yesu na familia yake!
Anakulinda pia!

Maandiko: Mathayo 2:13-18 (Mstari wa 13-15) Walipokwisha kwenda zao, malaika wa Bwana akamtokea Yosefu katika ndoto akamwambia, “Ondoka, mchukue mtoto na mama yake mkimbilie Misri. Kaeni huko mpaka nitakapowaambia, kwa maana Herode anataka kumtafuta huyu mtoto ili amuue.” Kisha Yosefu akaondoka, akamchukua mtoto pamoja na mama yake wakati wa usiku, nao wakaenda Misri ambako walikaa mpaka Herode alipofariki. Hili

©2010, Sharon Kay Chatwell

lilifanyika ili litimie lile lililonenwa na Bwana kwa kinywa cha nabii kusema: “Nilimwita mwanangu kutoka Misri.”

Mstari wa Kumbukumbu: Zaburi 121:5 BWANA atakulinda..…

Somo:

Krismasi ilikuwa ya furaha!!

- Krismasi ilikuwa ya kufurahisha mwaka huu! Niambie kuhusu Krismasi yako *(Subiri majibu. Acha kila mtoto azungumze.)*
- Hiyo inaonekana kama ya kufurahisha!
- Leo tutafurahi! Tutaenda kupiga kambi hapa chumbani! Lakini kwanza sina budi kukuambia hadithi kuhusu mtoto Yesu na familia yake.

Mungu anamtuma malaika kumwonya Yosefu kuhusu hatari fulani.

- Siku moja, baada ya Yesu kuzaliwa… na baada ya wachungaji kuja kumwabudu… na baada ya mamajusi kuja na kumwabudu… na kuleta zawadi zao zote… dhahabu, uvumba na manemane.… *(wooo ... hiyo ni mengi ya kusema ...)*
- Hata hivyo, siku moja baada ya yote kutokea, Yosefu alilala.
- Na usiku huo, Mungu alimtuma malaika kuzungumza na Yosefu katika ndoto yake.
- Malaika alimwambia Yosefu kwamba mtoto Yesu yuko hatarini!
- Kulikuwa na watu wabaya waliotaka kumuumiza mtoto Yesu.

Mungu aliwaambia wakimbilie Misri.

- Malaika alimuonya Yosefu ainuke, amchukue Maria na mtoto na kukimbilia Misri *(Misri ilikuwa nchi nyingine, iliyokuwa mbali sana.)*
- Mungu alijua kwamba wangekuwa salama huko Misri.

Yosefu alifanya kile ambacho Mungu alisema.

- Yosefu aliamka. Alifanya jinsi malaika alimwambia afanye.
- Alimwamsha Maria na wakamchukua mtoto Yesu na kukimbilia Misri.
- Waliondoka usiku na kwa haraka.

Bwana alimlinda Yesu na familia yake.

- Maria na Yosefu na mtoto Yesu walikuwa salama Misri.
- Walikaa huko kwa miaka kadhaa, mpaka Mungu alipomtuma tena malaika kwa Yusufu kumwambia wakati ambapo ilikuwa salama kurudi.
- BWANA alimlinda Yesu na familia yake.
- Na anakulinda pia!!

Ombi: Tuombe na kumshukuru Mungu kwa kuwa anatulinda!

Mungu Mpendwa,
Asante kwa kutulinda!
Asante kwa kumlinda mtoto Yesu na familia yake.
Asante kwa Krismasi.

Tunakupenda. Amina.

Shughuli Zilizopendekezwa: (Chagua shughuli zinazokufaa zaidi!)

Seti ya Krismasi - Kurasa za Kuchorea
Mpe kila mtoto kurasa za kuchorea za Krismasi na uwaambie wapambe kurasa ambazo bado hawajapamba. Tumia aina mbalimbali za kalamu za rangi, nk. Weka mashimo kwenye kingo za karatasi zote katika seti na uzifunge pamoja na vitanzi vya uzi ili kutengeneza kitabu cha kumbukumbu kutoka kwa mafundisho haya ya Krismasi.

Igiza Safari ya kuelekea Misri
Katika shughuli hii nzuri ya watoto wanajifanya kuigiza Safari ya Kukimbilia Misri wakiwa darasani… hadi kufikia kujenga “hema!” Utahitaji vitu vya kukusaidia kutengeneza "hema" katika darasa lako. ***(Njia rahisi ni kutupa mablanketi kadhaa au karatasi juu ya meza ndefu. Fanya mazoezi haya kabla ya darasa kuanza ama uache hema likiwa limejengwa au ulijenge upya wakati wa kuigiza.)*** Utahitaji pia kuwa na vitu ambavyo kawaida hubebwa wakati wa kupiga kambi au kusafiri. Mfano: chupa za maji; mkate au vitafunio vingine kavu, blanketi; na labda mkoba.

KUMBUKA: Ikiwa darasa lako lina watoto wengi, fikiria kugawanya katika vikundi kadhaa vidogo ili kusafiri pamoja, na Hema Ndogo kwa kila kikundi. Kuwa na mtu mzima mmoja kwa kila kikundi cha watoto 6-10 kwenye "hema". VINGINEVYO: Weka karatasi kubwa, au kipande cha kitambaa, kwa pembe zake kutoka kwenye dari kwenye kona moja ya chumba ili kuunda Hema Kubwa na darasa zima likae chini yake.

Anza kwa kuzungumza tu na watoto, kana kwamba somo bado linaendelea.

Safari ya kukimbilia Misri
- Yosefu, Maria na mtoto Yesu waliondoka Bethlehemu kwa haraka na katikati ya usiku.
- Walikuwa wanaenda safari ndefu.
- Ikiwa ungekuwa unaenda safari ndefu, ungechukua vitu vya aina gani?? *(Subiri majibu. Wanafunzi wanapotaja vitu ulivyo navyo kwa ajili ya kuigiza, vitoe nje na uviweke kwenye sakafu mbele yako.)*
- Hivi ni baadhi ya vitu ambavyo Maria na Yosefu wangebeba katika safari yao ya kwenda Misri. *(Waonyeshe watoto vitu vingine vyovyote ulivyo navyo. Jadili kwa nini wangebeba kila moja ya vitu hivi.)*

Anza Kuigiza
- Wacha tuigize tuko pamoja na Maria, Yosefu, na mtoto Yesu na kwamba lazima tukimbie na kujificha kutoka kwa askari wa Kirumi!
- Waliondoka katikati ya usiku. *(Fanya chumba kiwe giza kidogo.)*
- Chukua vitu vyote kwa haraka!! *(Gawa vitu vyote vya kubeba.)*
- Sawa, fanya haraka...Twende! *(Waongoze watoto kwenye "safari" kuzunguka chumba, ukisimama kwa muda mfupi mara*

kwa mara kwenye maeneo mbalimbali. Jifanye kuwaangalia walinzi wa Kirumi. Inama chini ili usionekane kwa urahisi. Ongea kwa minong'ono ya haraka. Hatimaye unafika mahali ambapo "utaweka kambi" na kupumzika.)

Kutengeneza Kambi/Hema na Vitafunio

- Tumetoka mbali sana! Nimechoka na nina njaa. Sioni walinzi wowote wa Kirumi kwa sasa. Labda tuko mbali vya kutosha na Bethlehemu ili tuwe salama kwa muda. Hebu tufanye kambi na tupate chakula na kupumzika. *(Weka hema kama ulivyofanya kabla ya darasa.)*
- Maria, Yosefu na mtoto Yesu wangekuwa na hema dogo kama hili la kupumzikia. Wangeweka vitu vyao vyote ndani hivi. *(Weka vitu kwenye hema. Tandika matandiko na kila mtu aketi ndani ya hema. Kila mtu anapokuwa ameketi, mega mkate na maji na kuleni vitafunio hemani!)*
- Maria na Yosefu na mtoto Yesu wangekuwa na chakula na maji. Maji ni muhimu sana huko, kwa sababu sehemu ya ardhi ni jangwa. (Unapokuwa na vitafunio hemani, zungumza na watoto kuhusu vipengele mbalimbali vya somo. Tumia muda na waache watoto wafurahie hema.)
    - Ingekuwaje kwa Maria, Yosefu na mtoto Yesu walipokuwa wakisafiri kujaribu kuwatoroka askari wa Kirumi?
    - Je, walipaswa kwenda na vitu vya aina gani?
    - Je, Mungu alimwonya vipi Yosefu kuhusu hatari iliyomkabili mtoto Yesu?
    - Mungu alimlinda mtoto Yesu na familia yake!
    - Mungu hutulinda sisi sote pia!
- Unapomaliza vitafunio vyako, weka takataka yako kwenye gunia hili. Watu wanaosafiri wanapaswa kusafisha. Hatuwezi kuacha alama yoyote kwamba tulikuwa hapa! Mtu anaweza kuipata na kutufuata! *(Waombe watoto wasaidie kusafisha.)*

Kwenda Misri… lakini kwanza…kulala kidogo!!

- Kazi nzuri, kusafisha! Lo, nina usingizi!! *(Piga miayo kwa sauti kubwa!)* Muda wa kupumzika kidogo kabla ya kuendelea! *(Lala na ujifanye unakoroma kwa nguvu. Keti baada ya muda mfupi au zaidi.)*
- Sawa ... huo usingizi unatosha! Tunapaswa kwenda! Askari hao wa Kirumi bado wanaweza kuwa nyuma yetu!
- Ondoa kambi. Kusanya kila kitu. Hatuwezi kuacha alama! (Kusanya bidhaa zote ulizokuja nazo. Pakia blanketi, vitafunio... hata takataka, ikiwa bado unayo.)
- Kwenda Misri! Twende!! *(Waongoze watoto nje ya hema na kuzunguka chumba tena hadi uishie "Misri".)*

©2010, Sharon Kay Chatwell

Kufika Misri.

- Hatimaye tuko Misri! Sasa tuko salama! *(Kaa chini.)*
- Maria na Yosefu na Yesu walikaa Misri kwa muda mrefu, mpaka watu wote waliotaka kumuumiza mtoto Yesu walipoondoka.
- Kisha Mungu akamtuma malaika kuwaambia kwamba ni salama kurudi.
- Walienda Nazareti, ambako waliishi hadi Yesu alipokuwa mtu mzima.
- Mungu alimlinda mtoto Yesu.
- Mungu anakulinda pia!!
- Vema… Maria, Yosefu na mtoto Yesu wako salama sasa! Ni wakati wa kuweka vitu vyetu! *(Washirikishe watoto katika kusafisha chumba na kukirejesha kama kinavyopaswa kuwa. Ondoa hema, weka vitu vyote, na utupe takataka!)*
  MWISHO